

Toleo la. 11

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | 10 SEPTEMBER, 2020



MAGUFULI ANG'ARA KILA KONA



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



SABABU ZA MVUTO WA KAMPENI ZA RAIS MAGUFULI, KUHUDHURIWA NA MAELFU YA WANANCHI

Na Mwandishi Wetu

Kumekuwa na maswali mengi juu ya kwa nini kampeni za Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli zimekuwa na mvuto na kukusanya umati wa watu katika maeneo yote, iwe barabarani au katika eneo lililoandaliwa maalum kwa ajili yakufanya mkutano wa kampeni.

Tangua azindue kampeni zake Agosti 29, 2020 katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, ambapo uzinduzi huo ulihudhuriwa na maelfu ya watu na kufanya wananchi wengine kusimama nje ya uwanja ili mradi tu wamehudhuria kampeni za mgombea huyo, hamasa ya kumuona Rais Magufuli akieleza utekelezaji wa kipindi cha miaka mitano na kunadi ilani kwa kipindi cha miaka mitano ijayo iliendelea katika kila sehemu alizopita.

01 | #NiMagufuliTena 2020 - 2025

Majibu ya maswali hayo ambayo wananchi na hata vyama vungine vya upinzani vime- kuwa vikijiuliza na kuweka mijadala, ni kwamba watanzania wanataka kuona utekelezaji, kusikia na kutaka kumuona Kiongozi ambaye kwa miaka mitano iliyopita alitoa ahadi na sasa ametekeleza na si viongozi ambao wananadi Sera wakati hawajawahi hata kutekeleza jambo moja.

Mgombea wa CCM, Rais Magufuli ametekeleza yale aliyoahidi kuyatekeleza wakati akiomba kura mwaka 2015 na hata zile changamoto ambazo hakuziahidi lakini alizitatua katika safari yake ya miaka mitano.

Rais Magufuli ametekeleza kwa vitendo katika kila sekta ikiwemo elimu ambapo ametoa elimu bila malipo kuanzia shule ya msingi mpaka kidato cha nne, ujenzi wa miundombinu kama barabara,



Reli ya kisasa ya SGR, Miradi ya umeme ya Kinyerezi II, Kinyerezi I Extension, Bwawa la kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), kuboresha huduma za afya ambapo amejenga hospitali za kanda, rufaa, hospitali za wilaya zaidi ya 97, vituo vya afya zaidi ya 480 ambapo ujenzi huo umeambatana na ununuzi wa vifaa tiba na vitendanishi pamoja na upatikanaji wa dawa.

Aidha, Rais Magufuli ameboresha sekta ya elimu kwa kujenga miundombinu ya shule, vyuo vya elimu, maabara pamoja na kuongeza fedha katika mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Pia ameweza kukabiliana kikamilifu na changamoto ya rushwa na ufisadi ambapo ameiimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kujenga mahakama za mafisadi ambapo kesi mbalimbali za mafisadi na wahujumu uchumi zinaendelea kusikilizwa, kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato pamoja na kufanya mabadiliko ya sheria ya madini ambayo imeleta mabadiliko makubwa katika sekta ya madini.

Katika miradi ya maji ametekelza ipasavyo ikiwemo mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ambao umefika Nzega, Igunga hadi Tabora. Mradi wa maji Longido na mradi wa maji Arusha wenye thamani ya shilingi bilioni 600 pamoja na miradi mingi ya maji nchi nzima. Aidha vijiji 9,570 vimekwisha vikishiwa umeme na kubaki vijiji 2600 tu ambavyo Mhe. Rais ameahidi kuvitekeleza katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Waswahili wanasema ukiona vinaelewa basi ujue vimeundwa, wananchi wanaviona jinsi vinavyoelea kwa sababu vimeundwa na ndiyo sababu kubwa ya wananchi wengi wanaji. tokeza katika mikutano ya kampeni ya Chama cha Mapinduzi hususan ya mgombea Urais Dkt, John Pombe Magufuli ili kwanza kumuona Mtekelezaji Mkuu wa Ilani na Ahadi lakini pia kusikiliza Ilani itakayoleta maendeleo zaidi kwa watanzania ambayo ataenda kuitekeleza kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Mpaka sasa Rais Magufuli kamapeni katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza na Geita. Katika ziara zake Mhe. Magufuli pia alisimama maeneo mbalimba ya vilaya na miji midogo kusalimia na kuongea na wananchi ambao walikuwa wanajikusanya kwa ajili ya kumsikiliza.



MTWARA WAMUAHIDI MAGUFULI USHINDI WA KISHINDO

Na Mwandishi Wetu - MTWARA

#NiMagufuliTena 2020 - 2025 | 02

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa wa Mtwara (CCM), Yusuf Nanila amesema wananchi wa mkoa huo watapiga kura zote za ndio kwa Mgombea wa Urais wa Chama hicho na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli Oktoba 28, 2020 kutokana na kazi nzuri inayofanyika na iliyoendelea kufanyika katika Sekta zote mkoani humo.

Nanila ameyasema hayo leo katika mkutano wa hadhara wa mgombea Mwezawa Urais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kuomba kura kwa wananchi wa jimbo la Nanyamba, mkoa wa Mtwara.

“Kujengwa kwa hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini kwa gharama ya bilioni 15 uliokuwa umekwama kwa miaka mingi kutawezesha wananchi wa mikoa hii kupata huduma bora za kibingwa kuanzia mwezi Oktoba 2020, huduma ambazo walikuwa wakizifuata Dar es Salaam,” amesisitiza Nanila.

Kwa upande wao wabunge akiwemo Abdallah Chikota anayegombea nafasi hiyo katika jimbo la Nanyamba amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa ikiwemo kutoa bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya na jengo la Halmashauri pamoja na kilomita 11 za lami zimejengwa.



MIRADI 49 YA MAJI IMETEKELEZWA

Kwa upande wa mradi wa maji, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Magufuli imetoa shilingi milioni 900 kugharamia mradi wa maji wa Nanyamba mjini na kwa upande wa umeme, vijiji 35 vimefikishiwa huduma ya umeme.

03 | #NiMagufuliTena 2020 - 2025

MKOANI MTWARA

Na Mwandishi Wetu - MTWARA

Jumla ya miradi 49 ya maji iliyogharimu shilingi bilioni 30.5 imetekelezwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na kuwanufaisha zaidi ya wananchi 257,220 katika mkoa wa Mtwara.

Hayo yamesemwa leo katika jimbo la Nanyamba na Mgombea Mwenza nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, wakati wa mkutano wake wa kumuomba kura Mgombea Urais, Dkt. John Pombe Magufuli, Wabunge na Madiwani ili wapewe ridhaa ya kuongoza Serikali kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Amesema kuwa kwa upande wa Mtwara vijijini upatikanaji umefikia asilimia 60.78 ikilinganishwa na lengo la asilimia 85 hivyo CCM ikipewa nafasi kwa awamu ya pili ya miaka mitano itakamilisha kiwango kilichobaki.

Kwa upande wa barabara Mama Samia alisema: “Barabara ya Mtwara Masasi yenye urefu wa kilomita 210 inajengwa kwa kiwango cha lami ambapo jumla ya kilomita 50 zilizogharimu shilingi



CHANGAMOTO YA UMEME MTWARA

bilioni 89 ujenzi wake uko katika hatua za mwisho kukamilika. Kama CCM itapewa ridhaa ya kuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo itakamilisha ujenzi wa barabara hiyo”.

Ameongeza kuwa bilioni 15.5 zimetolewa na Serikali ya Awamu ya Tano kutekeleza miradi ya maendeleo katika jimbo la Nanyamba mkoani Mtwara ikiwemo bilioni 3.2 za Sekta ya Afya na kwamba jumla ya shilingi bilioni 12.4 zimetolewa kwa Halmashauri zote ambapo ujenzi wa hospitali za Wilaya nne, zahanati 50 na Vituo vya Afya 11 umefanyika.

#NiMagufuliTena 2020 - 2025 | 04

YAPATIWA UFUMBUZI

Na Mwandishi Wetu

Changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika Mtwara Mjini imepatiwa ufumbuzi baada ya kufungwa kwa mashine mbili za kuzalisha umeme zenye uwezo wa kuzalisha megawati 10.

Hayo yamesemwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati wa mkutano wa hadhara wa kuomba kura kwa wananchi wa Mtwara Mjini leo Septemba 10, 2020 ambapo aliwahakikishia wakazi hao kuwa mitambo hiyo ya kuzalisha umeme iko katika majaribio na kufikia mwezi Oktoba changamoto hiyo itakuwa imeisha.

“Serikali iliiona changamoto hii hapa Mtwara Mjini hivyo umeme utakaozalishwa utaunganishwa na umeme unaozalishwa na mashine zilizopo ambazo zinalisha megawati 10 hivyo kufanya jumla ya umeme kufikia megawati 20, mahitaji ya mkoa huu ni megawati 16 hivyo tutakuwa na ziada,” alisisitiza Mhe. Samia.

Mgombea mwenza wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan anaendelea na mikutano ya kuomba kura kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara.

05 | #NiMagufuliTena 2020 - 2025

5 KALI ZA MAGUFULI KANDA YA ZIWA

01

Tumeboresha huduma za kibingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando kwa sasa wagonjwa wa moyo watakuwa wakihudumiwa hapa, tumejenga jengo la kuhudumia wagonjwa wa kansa na wagonjwa mahututi, kiwanda cha oksijeni na tumepeleka vifaa vya kisasa ikiwemo CT SCAN 128, Utra sound 12, Digital X- ray, radiotherapy na kujenga miundombinu mingine kwa gharama ya shilingi bilioni 11.4.

02

Tumejenga chujio la maji hapa wilayani Maswa kwa gharama ya shilingi bilioni 3.5.

03

Kuhusu miundombinu hapa Sengerema, tumekamilisha ujenzi wa gati la Mtama, tumejenga kivuko cha MV Mwanza , tumeendelea na ujenzi wa daraja la Busisi - Kigongo. Tumejenga vyote hivyo kwa fedha zetu, hatujakopa kwa mtu yeyote kwa sababu Tanzania ni tajiri.

04

Kutokana na mafanikio makubwa tuliyoyapata hasa kwa wachimbaji wadogo tumepanga kuhakikisha tunaimari-sha mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa



MAMA SALMA KIKWETE KUMALIZA TATIZO LA MAJI MCHINGA

kuwaongezea maeneo kuchimba madini, tutaendelea kuwapa leseni, mitaji na teknolojia rahisi ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Ni kwa mara ya kwanza Tanzania inafanya uchaguzi bila fedha za nje. Huko ndio kujitawala na kujitegemea. Ninaomba tuendeleo kusimama imara tukijua tuko kwenye mikono salama ya Chama cha Mapinduzi ambayo inatupeleka mahali pazuri ambapo nchi inakwenda kujitegemea.

Na Mwandishi Wetu - Mchinga - LINDI

Mgombea Mwenza wa Urais ambae pia ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewaomba wananchi wa jimbo la Mchinga Mkoani Lindi kumchagua Mama Salma Kikwete kuwa Mbunge wao kwani mgombea huyo ndiye atakayekuwa suluhisho ya tatizo la maji na changamoto zingine katika jimbo hilo.

“Nayasema haya kwa ushahidi kuwa mgombea aliyepatikana kwa nafasi ya Ubunge kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Salma Kikwete ameahidi kumaliza kabisa tatizo hili la maji, kazi kwenu wananchi wa jimbo hili kujitokeza kwa wingi kuchagua kilicho chema kwa manufaa yenu na vizazi vijavyo”, ameeleza Mhe. Samia alipokuwa akiongea na wananchi wa jimbo hilo kumuomba kura Mgombea Urais Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na mgombea Ubunge na Madiwani.

Makamu wa Rais amewataka wananchi wa jimbo la Mchinga wamchague Mhe. Salma Kikwete kuwa Mbunge wao ili aweletee maendeleo ya kweli tofauti na ilivyokuwa kwa kipindi cha miaka iliyopita ambapo walichagua Mbunge kutoka Upinzani lakini hakuweza kutimiza ndoto za wananchi wa jimbo hilo.

Kwa upande wake, Mgombea wa jimbo la Mchinga (CCM), Salma Kikwete, amesema miradi mbalimbali ya maendeleo

yametekelezwa ikiwemo elimu bure ambapo shilingi bilioni 2.7 zimetolewa na Serikali kugharamia elimu bure na kusababisha ongezeko la wanafunzi wa shule za msingi kutoka 40,760 hadi 46,348.

Pia zaidi ya shilingi milioni 400 zimetolewa kuboresha kituo cha afya Kitomanga na tayari upasuaji wa watu 300 umefanyika wakiwemo wajawazito 75 ambao wote wametoka salama wakiwa na watoto wao.

Jarida la **Ni Magufuli Tena**

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**